TANGAZO LA SERIKALI NA. 966 la tarehe 19/112024

SHERIA YA MISITU,

(SURA YA 323)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 23(1))*

NOTISI YA KUSUDIO LA KUTANGAZA ENEO LA MSITU WA SADANI KUWA MSITU WA HIFADHI WA TAIFA SADANI YA MWAKA 2024

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kusudio la Kutangaza Eneo la Msitu wa Sadani kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Sadani ya Mwaka 2024.

Eneo linalopendekezwa kutangazwa

2. Eneo la msitu lililo ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali linapendekezwa kutangazwa kama Msitu wa Hifadhi wa Taifa Sadani.

Madhumuni ya tangazo

3. Madhumuni ya kupendekezwa kutangaza Msitu wa Hifadhi wa Taifa Sadani ni-

(a) kulinda eneo lililo hatarini la misitu, nyasi na ardhi oevu ambalo linatambulika kwa thamani yake ya juu ya baioanuwai, lenye upekee wa mimea na wanyama, ikijumuisha aina za mimea na wanyama walio hatarini kutoweka; na

(b) kulinda eneo la msitu na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu katika eneo la msitu huo.

Uhalali wa Notisi

4.-(1) Notisi hii itakuwa halali kwa muda wa siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

(2) Ndani ya kipindi hicho cha siku tisini, mtu au

kundi la watu au mwakilishi wao anaweza, kwa maandishi kuwasilisha pingamizi, maoni au madai ya haki yoyote inayotokana na sheria za kimila kuhusiana na ardhi au mazao ya msitu au haki yoyote iliyoainishwa kwenye sheria nyingine katika eneo ambalo linapendekezwa kutangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Sadani.

Uwasilishaji wa pingamizi

5. Pingamizi, maoni au madai yoyote dhidi ya kusudio la kutangaza eneo la Msitu Sadani kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Sadani, yawasilishwe ndani ya siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa Notisi hii kwa anuani ifuatayo:

Katibu Mkuu,
Wizara ya Maliasili na Utalii,
S.L.P. 1351,
DODOMA.

*Tangazo la Serikali na. 966 (Linaendelea)*

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*


WILAYA YA MUFINDI

MSITU WA HIFADHI WA TAIFA SADANI

*Makadirio ya eneo: Hekta 8,122.6 au Kilometa za Mraba 88.22*

Unakopatikana na Mipaka:

Eneo lote la hifadhi awali chini ya Eneo la Msitu wa Sadani unaopatikana Wilaya ya Mufindi katika Mkoa wa Iringa kama lilivyochorwa katika Ramani Na. Jb 3091 (Skeli 1:50,000) iliyohifadhiwa na Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani na lenye mipaka ifuatayo:




Dodoma,
11 Novemba, 2024

PINDI HAZARA CHANA,
*Waziri wa Maliasili na Utalii*